



Huduma Maalumu na za Kina

MABADILIKO KWA HUDUMA KUTOKANA NA COVID-19

Huduma maalumu na za kina huendelea kuwasilishwa kwa wateja wakati wa mlipuko wa COVID-19. Hata hivyo, njia ambayo huduma zinawasilishwa zinaweza kubadilika kulingana na ushauri rasmi wa afya.

Tafadhali wasiliana na [mtoa huduma wako wako](#) moja kwa moja ili kujadiliana mipangilio mipya.

Jifunze kuhusu [COVID-19 na dalili zake \(symptoms\)](#)

Mapitio

Mpango wa Makazi ya Kibinadamu (HSP) hutoa Huduma Maalum na za Kina (SIS) kwa wahamiaji wa kibinadamu na wamiliki wengine wa viza wa stahili ambao wana mahitaji magumu.

SIS huwapa wateja msaada wa muda mfupi kulingana na mahitaji ili kuwasaidia kufikia huduma sahihi na kuendeleza ujuzi muhimu wa kusimamia mahitaji yao k kwa ujitegemea. SIS hutolewa na watoa huduma wa HSP kwa niaba ya Idara ya Mambo ya Ndani (Idara).

Maeneo ya watoa huduma za HSP na habari za mawasiliano [zinapatikana hapa](#)

Ustahili

Watu wenye viza moja ya hizi zifuatazo wanaweza kustahili kwa SIS:

- Wakimbizi (daraja 200, 201, 203 na 204)
- Maalum ya Kibinadamu ya Kimataifa (daraja 202)
- Ulinzi (daraja 866)
- Ulinzi wa Muda (daraja 785), Kukaa kwa Muda kwa kibinadamu (daraja 449), Suala ya Muda wa Kibinadamu (daraja 786) na Hifadhi Salama ya Biashara (daraja 790).

Wamiliki wa viza hizi wanaweza kuwa na haki kwa ajili ya SIS hadi miaka mitano baada ya kuwasili katika Australia, au hadi miaka mitano baada ya ruzuku ya viza yao ya stahifu ya nchi.

Katika hali ya kipekee, wamiliki wa viza hivi wanaweza kuwa na ustahili kwa SIS nje ya muda huu au ustahili unaweza kupanuliwa kwa wamiliki wa viza ndogo nyingine. Raia wa Australia hawastahiki kwa SIS.

Watu wanaostahili kwa ajili ya SIS wanapaswa kuonyesha kuwa hawawezi kujihusisha kuwa kujitegemea na msaada unaofaa na kuwa na vikwazo vingi au changamoto ambazo zinaweza kujumuisha:

- ulemavu
- mahitaji ya afya ambayo ni ya hali kali, muhimu, ya muda mrefu na/au yasiyosimamiwa
- masuala ya afya ya akili
- kukosa makazi au makazi yenye shida
- vurugu za ndani na za familia
- masuala ya ustawi wa watoto na vijana
- kuvunjika kwa familia na/au uhusiano
- kutengwa kwa jamii
- hali ngumu ya kifedha
- masuala ya kisheria

Nani anaweza kutuma mtu kwa SIS?

Shirika lolote au mtu yeyote anaweza kutuma mtu kwa SIS. Hii inajumuisha kujituma kwa kibinafsi.

Jinsi ya kupeleka mtu kwa SIS

Kumtuma mtu kwa SIS, tafadhali jaza fomu kwenye mtandao **Fomu ya Kumpeleka mtu kwa SIS**.

Ikiwa huna uhakika kama mtu anastahili kwa SIS, au kama unahitaji msaada wa kukamilisha fomu hii, tafadhali wasiliana na simu ya maswali ya SIS kwa kupiga simu kwenye 1300 855 669 wakati wa masaa ya biashara AEST (simu bure nchini Australia).

Ikiwa unapata matatizo ya kiufundi ili kukamilisha fomu ya mtandaoni, msaada unapatikana kwa kuwapiga simu HSP Msaada wa Mfumo wakati wa masaa ya ofisi kwa 1800 020 283 au kwa barua pepe hspsystem.helpdesk@dss.gov.au.

Kama huna uwezo wa kupata fomu mtandao unaweza kujaza **fomu ya karatasi**.

Inatokea nini baada ya kuwa rufaa ikishawakilishwa

Mara tu Idara inapokea fomu iliyokamilika, itatathmini ustahili wa mtu huyo inajulikana na kuarifu yule aliyemtuma juu ya uamuzi huo. Ikiwa mtu huyu akipatikana na kustahili na vigezo vya kustahiki kwa SIS, Idara itajihusisha na Mtoa Huduma wa HSP ili kutoa SIS kwa mtu.

Urefu wa muda ambao mteja anapokea SIS unategemea na mahitaji binafsi, lakini kwa kawaida itakuwa hadi miezi sita.